**HOTUBA YA SIKU MIA MOJA (100) ZA MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA (MB.) TOKA ALIPOTEULIWA NA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUWA WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI LEO TAREHE 22 DISEMBA, 2023 KATIKA UKUMBI WA KIMATAIFA WA MIKUTANO WA MWALIMU NYERERE JIJINI DAR ES SALAAM**

**Mhe. Geophrey Mizengo Pinda (Mb.), Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

**Mhe. Timotheo Mnzava, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii,**

**Eng. Anthony Sanga, Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,**

**Bibi Lucy Kabyemera, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi,**

**Ndugu Nathaniel Mathew Nhonge, Kamishna wa Ardhi,**

**Ndugu Hamad Abdallah, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba,**

**Prof. Wakuru Magigi, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi,**

**Ndugu Nevline Meena, Kaimu Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri,**

**Wakuu wa Vyuo vya Ardhi Tabora na Morogoro,**

**Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara,**

**Makamishna wa Ardhi Wasaidizi wa Mikoa Mliofika,**

**Watendaji wote wa Wizara,**

**Viongozi na Wajumbe wa Jukwaa la Wahariri,**

**Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake,**

**Wahariri wa Habari,**

**Waandishi wa Habari,**

**Mabibi na Mabwana,**

***"JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA***

***Kazi Iendelee"***

**Ndugu Wanahabari,** awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ameendelea kunijalia uhai na afya njema vinavyoniwezesha kutekeleza majukumu yangu hadi sasa. Kipekee, ninamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshmiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani yake aliyoionesha kwangu na kuniteua kuwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**Ndugu Wanahabari,** mtakumbuka kuwa tarehe 30 Agosti, 2023, Rais wa Jamhuri wa Tanzania, Mheshmiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliniteua na kunipa dhamana ya kuiongoza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama Waziri. Aidha, tarehe 1 Septemba, 2023 katika Ikulu Ndogo ya Tunguu Zanzibar, aliniapisha na kunikabidhi rasmi majukumu ya

kuiongoza Wizara hii. Imani hii ambayo Mheshimiwa Rais aliionesha kwangu ni kubwa na nimeendelea kuitunza wakati wote wa utekelezaji wa majukumu niliyopewa.

**Ndugu Wanahabari,** baada ya kuteuliwa na kuapishwa kama Waziri mwenye dhamana na Sekta ya Ardhi, tarehe 04 Septemba, 2023 nilipata fursa ya kuingia kwa mara ya kwanza Ofisi Jijini Dodoma ambapo pia nilipata fursa ya kuzungumza na watumishi na menejimenti nzima ya Wizara. Katika kikao hicho, pamoja na mambo mengine nilianisha vipaumbele 12 ambavyo vitakuwa ni sehemu ya misingi ya utendaji kwa kipindi chote cha uongozi wangu kama Waziri. Aidha, nilitoa muda wa siku mia moja (100) kwa watendaji wa Sekta ya Ardhi nchini kutekeleza kwa vitendo vipaumbele hivyo.

**Ndugu Wanahabari,** tarehe 13 Disemba, 2023 nilitimiza siku 100 toka nilipoanza kazi rasmi kama Waziri. Nipende kuwafahamaisha kuwa kwa kipindi chote hiki, nimepata muda wa kutosha wa kujifunza, kuzunguka kwenye maeneo mbalimbali, kufanya mikutano, na kushughulika kwa kiasi kikubwa na majukumu yangu kama Waziri. Aidha, nimepata fursa ya kufahamu maeneo yenye changamoto na yanayohitaji maboresho makubwa ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa ufanisi mkubwa.

**Ndugu Wanahabari**, ikiwa ni siku mia moja toka nianze kazi kama Waziri wa Ardhi nimeweza kuzunguka katika mikoa 25 kati ya 26 iliyopo Tanzania Bara. Aidha, nimetembea jumla ya kilomita **35,899**, kilomita **13,786** zikiwa ni kwa njia ya barabara na **22,113** ni kwa njia ya anga. Vilevile, kwa siku zote hizo nimetumia jumla ya **masaa 219 na dakika 09** sawa na **siku 9 na**

**masaa 13** kusikiliza na kutatua kero za wananchi; kufuatilia utekelezaji wa uamuzi wa BLM pamoja na kukagua utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwenye mikoa.

**Ndugu Wanahabari, mtakumbuka kuwa tarehe 04 Septemba, 2023 nilieleza azma yangu ya kushughulikia migogoro ya ardhi ndani ya siku hizi mia moja**. Ili kutekeleza azma hii, niliwaelekeza watendaji wangu kote nchini kuhakikisha kuwa migogoro yote kwenye ameneo yao inatatuliwa na kufungwa. Aidha, nilipewa maelekezo mahsusi na Mhe. Rais kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Uamuzi wa Baraza la Mawaziri (BLM) kuhusu migogoro ya ardhi katika vijiji 975 nchini.

**Ndugu Wanahabari,** napenda kuwafahamisha kuwa kwa kipindi chote hicho nimefanikiwa kuzunguka katika mikoa **25** kati ya **26** iliyopo isipokuwa Mkoa wa Ruvuma pekee kufuatilia utekelezaji wa uamuzi wa BLM kuhusu migogoro katika vijiji 975 pamoja na utekelezaji wa majukumu mengine ya Wizara. Katika mikoa niliyofanya ziara ipo ambayo nilipita zaidi ya mara moja kama **Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Singida, Tabora, Katavi, Rukwa, Mbeya, Lindi, Mtwara, Pwani, Kilimanjaro, Manyara, Shinyanga, Mwanza na Njombe.** Aidha, nimejiridhisha kuwa uamuzi huo wa BLM umetekelezwa kwa kiwango kikubwa kwa usimamizi mahiri wa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa. **Napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa kote nchini kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia utekelezaji wa uamuzi huo katika mikoa, na nitoe rai kwao kuendelea kusimamia ukamilishaji wa kazi zilizobakia.**

**Ndugu Wanahabari,** niwahakikishie kuwa kwa kiasi kikubwa migogoro mikubwa yenye athari kwa watu wengi imetolewa uamuzi na kupatiwa

ufumbuzi na Serikali. Aidha, shilingi **bilioni 178 zitalipwa** kama fidia kwa wananchi ambao watapisha maeneo yaliyohifadhiwa kwa matumizi mbalimbali. Kwa migogoro inayogusa watu wachache au mtu mmoja mmoja, Wizara imeendelea kuitatua kwa kuendesha kliniki za ardhi katika maeneo yote kwa lengo la kuipatia ufumbuzi wa haraka.

**Niwaelekeze Makamishna wa Ardhi Wasaidizi kote nchini, kuhakikisha kuwa kliniki hizi zinaendelea kuendeshwa nchi nzima na wananchi wote wenye kero mbalimbali za ardhi wafike kupata majibu ya kero zao. Aidha, nimekwishamwelekeza Katibu Mkuu na nitatambua tayari ameanza kusimamia na kuratibu ratiba za kliniki zinazoendelea katika mikoa yote na niwahakikishie kuwa sisi viongozi wakuu wa Wizara tutaendelea kushiriki kikamilifu.**

**Ndugu Wanahabari**, ninatambua kuwa wananchi wameendelea kuwasilisha kero na malalamiko yao kwangu. Kwa kipindi chote kama Waziri nimepokea takriban barua **587** za malalamiko ya wananchi kutoka katika maeneo mbalimbali nchini. Niwafahamishe kuwa asilimia kubwa ya malalamiko hayo siyo mapya na yamekuwa yakiwasilishwa mara kwa mara Wizarani hususani pale inapotokea mabadiliko ya kiongozi. **Niwahakikishie wananchi wote waliowasilisha kwangu malalamiko kwa njia yoyote ikiwemo ya barua, baadhi ya malalamiko yao yamepatiwa ufumbuzi na mengine yanaendelea kushughulikiwa. Niwahimize watendaji wote wa Wizara kuhakikisha wanatolea majibu malalamiko na kero zote zinazowasilishwa katika kila ngazi yao ya maamuzi.**

**Ndugu Wanahabari**, Wizara inakusudia kufanya mageuzi makubwa ya kimfumo wa utendaji katika Sekta ya Ardhi nchini. Mageuzi hayo yanalenga kuboresha utendaji kazi katika utoaji huduma za sekta ya ardhi. Mageuzi hayo ni pamoja na masuala yafuatayo: -

**a)** Kufanya mabadiliko ya Kisera, Kisheria na Kikanuni ili kukidhi mahitaji yaliyopo kwa sasa na baadaye. Nipende kuwafahamisha kuwa marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 yamepata kibali cha Serikali na kwa sasa tunaendelea na taratibu za ukamilishaji wa mchakato huo ikiwemo kuzinduliwa rasmi. Mabadiliko hayo ya Kisera, yatasababisha kubadilishwa kwa Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta ya Ardhi nchini;

b) Kuboresha Programu ya Kupanga, Kupima, Kumilikisha ardhi (KKK) kwa kushirikisha pia Sekta Binafsi na Mamlaka za Upangaji. Katika maboresho haya tutafanya marekebisho ya utaratibu wa kukopesha fedha kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja (Plot Development Revolving Fund – PDRF) utakaokuwa unatunza fedha na kukopesha fedha kwa ajili ya KKK;

c) Mtakumbuka kuwa nilisitisha matumizi ya Kanuni za Viwango vya Nafasi pamoja na za Matumizi ya Ardhi za Mwaka 2018 kutokana na kuongezeka kwa kasi ya mabadiliko ya matumizi kwa ajili ya vituo vya mafuta, ukubwa wa mashamba ya mijini na mambo mengine yanayoleta kero kwa wananchi. Wizara inakusudia kufanya maboresho ya Kanuni hizo ambazo pamoja na mambo mengine tunakusudia kuweka masharti ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi kupata idhini ya Katibu Mkuu/Waziri kupitia KU za Wilaya na Mikoa;

d) Kuondoa mamlaka ya Halmashauri kusimamia maeneo ya wazi na umma na kurejesha mamlaka hiyo Serikali Kuu (Wizarani);

e) Kuandaa utaratibu mpya wa kuzitaka Taasisi zinazotwaa ardhi kulipa fidia katika akaunti maalum (escrow account) baada ya uthamini wa makadirio kufanyika kabla ya uthamini halisi. Miradi ya kimkakati haitahusika katika utaratibu huu baada ya kupata idhini aya Mhe. Rais.;

f) Kukamilisha maboresho ya mfumo wa TEHAMA ambao utaruhusu huduma na miamala ya Sekta kuanza kutolewa kidigitali. Tunarajia mfumo huu utaanza kutumika hivi karibuni kwa kuanza na mikoa ya Arusha, Tanga, Mwanza na Mbeya. Sambamba na hatua hii, leo tutazindua rasmi mfumo wa **ARDHI KLINIKI KIGANJANI** maalumu itakayowezesha kupokea na kushughulikia malalamiko yote yatakayowasilishwa kiurahisi kwa kutumia simu ya kiganjani au kompyuta;

g) Mabadiliko ya kimuundo na ya kiutendaji ikiwemo kuanzisha mikoa maalumu ya ardhi katika maeneo yenye uhitaji mkubwa na kwa kuanzia tumeanza na Mkoa wa Dodoma na Dar es Salaam, maboresho hayo yanaweza kuendelea kufanyika katika mikoa yenye miamala mingi ya ardhi ikiwemo Mkoa wa Mwanza na Pwani.

h) Kuboresha mfumo wa usimamizi wa watendaji wa Sekta hadi ngazi za chini kama sehemu ya utekelezaji wa marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 na Sheria zake;

i) Kuimarisha utendaji kwa kusimamia taaluma pamoja na mwenendo wa kampuni binafsi zinazotoa huduma za ardhi ili kuepukana na vitendo vya ukosefu wa maadili miongoni mwa watendaji na

kampuni hizo. Kwa kuanzia, Wizara imewachukulia hatua baadhi ya Watendaji na Kampuni zilizobainika kukiuka maadali ya utendaji na kusababisha migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini;

j) Kuweka mpango wa kupanga na kupima ardhi na baadaye umilikishaji kwa matumizi mahsusi na kuweka ardhi ya uwekezaji na Hazina ya Ardhi;

k) Kupitia upya Mradi wa Uboreshaji wa Milki za Ardhi (LTIP) kwa kujadiliana na WB ili kuongeza idadi ya vijiji vitakavyoandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi;

l) Kuendelea kuendesha kliniki za ardhi katika mikoa yote nchini kwa kuwa kliniki hizi zimekuwa na faida kubwa kwa kuongeza kasi ya utoaji huduma, kusogeza huduma kwa wananchi, kupunguza gharama, kuongeza makusanyo ya maduhuli ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Ardhi pamoja na kutatua migogoro ya ardhi;

m) Kuchukua hatua kwa migogoro ya ardhi inayotokana na uvamizi wa kijinai (Mfano migogoro sugu ya ardhi Mapinga – Bagamoyo, Pangani – Kibaha, Mabwepande – Ubungo, Ndachi, Mbuyuni na Kizota – Dodoma, n.k); na

n) Udhibiti wa ujenzi holela wa viwanda na kuelekeza viwanda kujengwa katika maeneo ya kongani za Viwanda. Mtazamo wa Wizara, ni kuongeza maeneo ya kutosha kwa ajili ya Kongani za Viwanda mathalani Kongani ya Viwanda Kamaka iliyopo Mlandizi na Kwala iliyopo Chalinze na SinoTan katika eneo la Kibaha;

o) kuweka chombo cha uthibiti wa Sekta ya Milki (Real Estate Regulatory Authority - RERA ambacho kitasimamia sekta ya milki

pamoja na wadau wote muhimu. Maboresho haya yanalenga kukabiliana na changamoto zinazoikabili Sekta ya Milki zinazohusiana na upatikanaji wa fedha za uendelezaji milki; waendelezaji na hasa kwenye sekta ya Nyumba; na Wadau wengine wakiwemo mawakala, madalali wauzaji na wanunuzi/wapangaji.

**Ndugu Wanahabari**, nilijipa siku hizo mia moja kwa lengo la kuifahamu vizuri Wizara, kuweka utaratibu mzuri wa utendaji na kuainisha maeneo muhimu yanayohitaji mageuzi kama nilivyoeleza. Mwelekeo sasa ni kusimamia mageuzi hayo kwa vitendo kwa kushirikiana na wadau wote muhimu mkiwemo ninyi Jukwaa la Wahariri. **Niwaombe muwe kiungo muhimu kati ya Wizara na Wananchi ili kutusaidia kufanikisha malengo haya tuliyojiwekea pamoja na kumsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye matumaini yake muda wote ni kuona changamoto za ardhi zinatatuliwa na kuifanya ardhi kuwa mkombozi wa Maisha ya Watanzania.**

**Ndugu Wanahabari,** mwisho na kwa mara nyingine tena nimshukuru Mhe. Rais kwa namna anavyoendelea kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake. Aidha, niwashukuru viongozi wengine wote na Wananchi kwa ujumla kwa namna wanavyoendelea kutoa ushirikiano wao kwetu katika mazingira yoyote yanayojitokeza. Mwisho, ila siyo kwa umuhimu niwashukuru sana Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Viongozi wa CCM na Watendaji wote Sekta ya Ardhi katika ngazi zote kwa namna wanavyopambana kuhakikisha kuwa Wizara inafikia malengo yake

iliyojiwekea ikiwemo kukabiliana na kero za ardhi. Niwaahidi kuwapa ushirikiano wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yangu.

**Ndugu Wanahabari**, baada ya kusema hayo sasa nitamke rasmi kuwa nipo tayari pia kuzindua mfumo wa ***ARDHI KLINIKI KIGANJANI*** pamoja na kuendelea na ratiba inayofuata.

***JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA***

***Kazi Iendelee***

***Jerry William Silaa (Mb.)***

***WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI***